

# 2023

## TCCIA INVESTMENT PLC

MKUTANO MKUU WA
18 WA WANAHISA 05/08/2023



# TAARIFA YA KAMPUNI

Kwenye Mkutano Mkuu wa 18 wa Wanahisa

## TAARIFA YA KUITISHA MKUTANO NA AKIDI

Wanahisa wanaombwa kuzingatia taarifa iliyotolewa kulingana na kifungu Namba 33 cha Kanuni za Kampuni kinachohusu uitishaji wa Mkutano Mkuu wa Wanahisa.

Wanahisa wanaombwa kuzingatia kuwa, akidi kwa mujibu wa kifungu Na. 38 cha Kanuni za Kampuni ni idadi ya wanahisa wasiopungua 10 wanaomiliki hisa zaidi ya asilimia 50.

### TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA KUMI NA NANE

UTAKAOFANYIKA SIKU YA JUMAMOSI TAREHE 05 Agosti 2023.
Tunapenda kukujulisha kuwa Mkutano Mkuu wa kumi na nane wa Wanahisa wa TCCIA Investment PLC, utafanyika siku ya Jumamosi tarehe 05 Agosti 2023 kwa njia ya mtandao.

Dondoo Na. 18/1/2023

# KUPOKEA AJENDA

Wanahisa mnaombwa kupokea Ajenda kama zilivyowasilishwa.



Dondoo Na. 18/2/2023

# TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA KUMI NA NANE UTAKAOFANYIKA SIKU YA JUMAMOSI TAREHE 05 AGOSTI 2023.

Tunapenda kukujulisha kuwa, Mkutano Mkuu wa Kumi na Nane wa Wanahisa wa TCCIA Investment PLC, utafanyika siku ya Jumamosi tarehe 05 Agosti 2023 kwa njia ya mtandao. Mkutano utaanza saa Tatu kamili (3:00) asubuhi. Kampuni itawatumia Wanahisa wote kupitia simu zao za mkononi utambulisho na maelekezo kuhusu jinsi ya kujiunga na kushiriki Mkutano Mkuu kidigitali.

**Dondoo za Mkutano Mkuu wa Kumi na Nane ni:**

1. Kufungua Mkutano Mkuu wa Kumi na Nane;
2. Kupokea na kuridhia Dondoo za Mkutano Mkuu wa Kumi na Nane;
3. Kuthibitisha Kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Kumi na Saba;
4. Yatokanayo na Mkutano Mkuu wa Kumi na Saba;
5. Kupokea, kujadili na kuridhia Taarifa ya Wakurugenzi wa Bodi ya Kampuni na Taarifa ya Mahesabu yaliyokaguliwa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 31 Desemba, 2022;
6. Kupokea, kujadili na kuridhia pendekezo la Bodi kuhusu Malipo ya Gawio kwa Mwaka 2022;
7. Kupokea, kujadili na kuridhia pendekezo la Bodi kuhusu uteuzi wa Mkaguzi wa Mahesabu ya Kampuni kwa Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 31 Desemba, 2023;
8. Kupokea, kujadili na kuridhia pendekezo la Bodi kuhusu Malipo ya Wajumbe wa Bodi;
9. Kupokea, kujadili na kuridhia pendekezo la kubadilisha jina la Kampuni;
10. Kupokea, kujadili na kuamua mapendekezo kutoka kwa Wanahisa;
11. Kufunga Mkutano Mkuu wa Kumi na Nane.

**Maelezo:**

1. Mapendekezo yote kutoka kwa wanahisa yatakayojadiliwa katika dondoo namba 10 yatumwe na kumfikia Katibu kabla ya tarehe 14/07/2023;
2. Taarifa ya Mwaka 2022 na Makabrasha ya Mkutano itapatikana kwenye tovuti ya Kampuni *(https://www.tcciainvest.co.tz)* kuanzia tarehe 21/07/2023;
3. Endapo Mwanahisa atashindwa kuhudhuria anaombwa, kuteua Mwakilishi atakayehudhuria Mkutano kwa niaba yake. Fomu ya Uwakilishi inapatikana kwenye tovuti ya Kampuni *(https:// www.tcciainvest.co.tz)*. Fomu za Uwakilishi zilizojazwa zitumwe kwa Katibu kupitia barua pepe *info@tcciainvest.co.tz* au picha ya fomu ya uwakilishi iliyojazwa itumwe kwenye WhatsApp na. 0757-138048 na kumfikia Katibu kabla ya tarehe 04/08/2023. saa kumi kamili jioni.

Imetolewa kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi.

**Peter W. Kifunguomali**
Katibu
Tarehe: **02/07/2023**

# KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA KUMI NA SABA WA WANAHISA ULIOFANYIKA SIKU YA JUMAMOSI, TAREHE 5 NOVEMBA, 2022 KWA NJIA YA MTANDAO.

## 17.1 WALIOHUDHURIA

| | | |
|---|---|---|
| 1. Bw. Fortunatus Magambo | - | Mwenyekiti |
| 2. Bw. Peter W. Kifunguomali | - | Katibu |
| 3. Prof. Lucian A. Msambichaka | - | Mjumbe wa Bodi |
| 4. Bw. Joseph M. Kahungwa | - | Mjumbe wa Bodi |
| 5. Bi. Magdalene N. E. Mkocha | - | Mjumbe wa Bodi |
| 6. Bw. Nathan E. Mnyawami | - | Mjumbe wa Bodi |
| 7. Bw. Ernest R. Khisombi | - | Mjumbe wa Bodi |
| 8. Bw. Paul F. Koyi | - | Mjumbe wa Bodi |

### WANAHISA WAKUU

1. Public Service Social Security Fund
2. Mkombozi Fishing & Maring Transport Ltd
3. Abbasi Exports Limited
4. Christopher Mwita Gachuma
5. Nimrod Elireheemah Mkono

Orodha ya Wajumbe pamoja na Wawakilishi wa Wanahisa waliohudhuria Mkutano Mkuu wa Kumi na Saba uliofanyika siku ya Jumamosi tarehe 5 Novemba, 2022 imeambatanishwa kwenye Kumbukumbu hizi. Tafadhali angalia Kiambatisho Namba 1.

## 17.2 KUFUNGUA MKUTANO MKUU WA KUMI NA SABA

Mwenyekiti alifungua Mkutano kwa kuwakaribisha Wanahisa, Wajumbe wa Bodi, Wageni Waalikwa na Wafanyakazi wa Kampuni kwenye Mkutano Mkuu wa 17 wa Mwaka. Baada ya Kutolewa taarifa kwamba Akidi ilikuwa imetimia kulingana na Kifungu Namba 38 cha Kanuni za Kampuni, Mwenyekiti alifungua Mkutano saa 3:08 Asubuhi.

## 17.3 KUPOKEA NA KURIDHIA DONDOO ZA MKUTANO MKUU WA KUMI NA SABA.

Hakukuwa na Mabadiliko yoyote hivyo Wajumbe walipitisha Dondoo za Mkutano Mkuu wa Kumi na Saba kama zilivyoainishwa kwenye ajenda.

## 17.4 KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA KUMI NA SITA.

Wajumbe walithibitisha Kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Kumi na Sita na zikasainiwa na Mwenyekiti na Katibu.

## 17.5 KUPOKEA, KUJADILI NA KURIDHIA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA MKUTANO MKUU WA KUMI NA SITA ULIOFANYIKA TAREHE 20 NOVEMBA, 2021.

Taarifa ilitolewa utekelezaji wa maazimio mbalimbali yaliyopitishwa na Wajumbe wakati wa Mkutano Mkuu wa Kumi na Sita uliofanyika tarehe 20 Novemba, 2021 na kukubaliwa na Wanahisa.

## 17.6 KUPOKEA, KUJADILI NA KURIDHIA TAARIFA YA WAKURUGENZI WA BODI YA KAMPUNI KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TARE HE 31 Desemba, 2021.

17.6.1.5 Mwenyekiti aliwajulisha wajumbe kuwa, Kampuni imeshachukua hatua ya kuwekeza katika vyanzo vingine vya mapato kama dhamana za serikali za muda mrefu na mfupi.

## 17.7 KUPOKEA, KUJADILI NA KURIDHIA TAARIFA YA MAHESABU YA KAMPUNI YALIYOKAGULIWA KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 31 Desemba, 2021.

Taarifa ya Mahesabu iliwasilishwa na haikukinzana na taarifa nyingine. Kulingana na Taarifa ya mahesabu, shughuli za Kampuni zitaendelea bila kuathiriwa na chochote. Mkaguzi wa Mahesabu aliwajulisha wajumbe kuwa, Kwa mwaka wa fedha wa 2021, Kampuni Ilipata Hati safi. Iliazimiwa kwamba Taarifa ya mahesabu ya Kampuni yaliyokaguliwa kwa kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2021 yamepitishwa kama ilivyowasilishwa.

## 17.8 AZIMIO KUHUSU MALIPO YA GAWIO

Bodi ilipendekeza kuwa malipo ya gawio kwa wanahisa yafanyike siku tisini (90) baada ya kupitisha azimio.

Kwa Wanahisa ambao wana akaunti za benki malipo yatalipwa kupitia kwenye akaunti zao na kwa njia ya mitandao ya simu.

Mkutano Mkuu uliazimia na kuridhia gawio la shilingi za Kitanzania (10) kwa kila hisa kama ilivyopendekezwa na Bodi ya Wakurugenzi.

## 17.9 UTEUZI WA MKAGUZI WA MAHESABU YA KAMPUNI KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA DESEMBA 31, 2022

Bodi ilipendekeza kuwa, CROWE Tanzania wateuliwe tena kukagua Mahesabu ya Kampuni kwa mwaka unaoishia Desemba 31, 2021. Ada ya Ukaguzi iliyopendekezwa ni kiasi cha Shilingi 20 milioni kabla ya VAT. Ilielezwa kuwa ada inayopendekezwa na Bodi imezingatia mwenendo wa Soko kwa taaluma ya Uhasibu na Ukaguzi, ukuaji wa shughuli za Kampuni na mfumuko wa bei nchini.

Iliazimiwa kukubaliana na pendekezo la Bodi ya Wakurugenzi kuwa CROWE Tanzania waendelee kukagua Mahesabu ya Kampuni kwa Mwaka wa Fedha unaoishia Desemba 31, 2022. Pamoja na kuidhinisha Shilingi 20 milioni kabla ya VAT kama gharama za malipo ya ukaguzi wa mahesabu ya Kampuni.

## 17.10 PENDEKEZO KUHUSU MALIPO YA WAKURUGENZI

Mkutano Mkuu uliarifiwa kwa kuzingatia matokeo ya shughuli za Kampuni kwa Mwaka wa fedha ulioishia Desemba 31, 2021, Menejimenti ilipendekeza kuwa Wajumbe wa Bodi walipwe Shilingi milioni nne na laki nane (Shilingi 4,800,000), kama ilivyokuwa mwaka jana.

Iliazimiwa kwamba kama ilivyopendekezwa na Menejimenti, malipo ya Wakurugenzi wa Bodi yawe Shilingi milioni nne na laki nane (Shilingi 4,800,000) kwa kila Mjumbe wa Bodi.

17.6.1 Wanahisa walipokea taarifa za mwenyekiti wa Bodi, Mkurugenzi Mtendaji na hesabu zilizokaguliwa na kujadi kama ifuatavyo

17.6.1.1 Majadiliano kutoka kwa Wanahisa ni kama ifuatavyo;

17.6.1.2 Walipongeza Bodi ya Wakurugenzi kwa Taarifa nzuri;

17.6.1.3 Ni vema Bodi iendelee kuangalia namna ya kuongeza mapato ya Kampuni na kuepuka matumizi yasiyo ya lazima;

17.6.1.4 Kuangalia fursa mbalimbali katika uwekezaji katika sekta nyingine;

### 17.11 PENDEKEZO LA KUORODHESHA HISA ZA KAMPUNI KWENYE SOKO LA HISA LA AFRINEX-MAURITIUS (CROSS-LISTING)

Mkutano Mkuu uliarifiwa kwamba, Bodi inapendekeza kuorodhesha Kampuni yetu kwenye soko la Kimataifa la Dhamana na Mitaji AFRINEX nchini Mauritius (Cross listing) amabalo ni lango la kupanua wigo wa kukutanisha watoa Mitaji wa Africa na Duniani kote.

Mkutano Mkuu iliombwa kuridhia Pendekezo hili baada ya kukamilisha hatua zinazotakiwa kwenye Soko la Hisa la Kimataifa Mauritius pamoja na kurekebisha maeneo ya Katiba ambayo yataonekana yanahitaji kufanyiwa marekebisho ili kukidhi matakwa ya Sheria na Kanuni za Mamlaka husika.

Mkutano mkuu uliazimia kwamba kama ilivyopendekezwa na Bodi Kampuni iorodheshe hisa zake kwenye soko la Hisa AFRINEX- MAURITIUS (CROSS-LISTING).

### 17.12 KUPOKEA, KUJADILI NA KURIDHIA PENDEKEZO LA KAMPUNI KUNUNUA BAADHI YA HISA ZAKE (SHARE BUY BACK)

Mkutano Mkuu uliarifiwa kwamba, kwa miaka kadhaa Menejimenti imekuwa ikipokea malalamiko kutoka kwa wanahisa ambao wanahitaji kuuza hisa zao, lakini wakashindwa kutokana na kukosekana kwa wanunuzi. Taarifa za Soko la Hisa za hivi karibuni zinaonyesha kuwa kulikuwa na hisa 140,000 ambazo hazijanunuliwa.

Bodi ilipendekeza kuwa, Kampuni itenge shilingi milioni mia moja kwa kila mwaka mfulilizo kwa miaka mitatu kulingana na bei ya soko ili kuweza kunua hisa.

Iliazimiwa kwamba Kampuni itenge shilingi milioni mia moja kwa kila mwaka mfulilizo kwa miaka mitatu kulingana na bei ya soko ili kuweza kunua hisa kama ilivyopendekezwa na bodi ya Wakurugenzi.

### 17.13 KUFUNGA KWA MKUTANO MKUU WA KUMI NA SABA

Mwenyekiti wa Bodi aliwashkuru wanahisa wote, Wajumbe wa Bodi, Wafanyakazi pamoja na wageni waalikwa wote kwa kuhudhuria Mkutano Mkuu wa 17 pamoja na mchango wao katika kuboresha maendeleo ya Kampuni.

Mkutano ulifungwa saa 4:10 Asubuhi

| | |
|---|---|
| ........................................................ | ........................................................ |
| **Katibu** | **Mwenyekiti** |
| Tarehe: | Tarehe: |

Dondoo Na. 18/3/2023

## KUTHIBITISHA MUHTASARI WA MKUTANO MKUU WA KUMI NA SABA WA MWAKA ULIOFANYIKA TAREHE 05 NOVEMBA, 2022

### WASILISHO

Wanahisa wanaombwa kupokea na kuthibitisha Muhtasari wa Mkutano Mkuu wa 17 uliofanyika tarehe 05, Novemba, 2022 kama kumbukumbu sahihi:-

> **"Azimio la 1/2023**
>
> Imeazimiwa kuwa Muhtasari wa Mkutano Mkuu wa kumi na Saba ulifanyika tarehe 05 Novemba, 2022 ni kumbukumbu sahihi"


# YATOKANAYO NA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU ULIOPITA

*Jedwali na. 1*

| Kumb | Maelezo mafupi | Azimio | Utekelezaji |
|---|---|---|---|
| **17.8** | Malipo ya Gawio | Gawio lilipwe Shilingi Kumi (10) kwa kila hisa moja. | Limetekelezwa kwa wale ambao taarifa zao zimekamilika. Wamelipwa magawio yao tarehe 7/11/2022. |
| **17.9** | Kuteua Mkaguzi wa Mahesabu | Mkutano Mkuu uliidhinisha CROWE Tanzania kukagua Mahesabu ya Kampuni kwa Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 31 Desemba, 2022. | Limetekelezwa. Kampuni ya Crowe Tanzania ndio wakaguzi wa nje wa hesabu kwa mwaka 2022. |
| **17.10** | Malipo ya Wakurugenzi | Wajumbe wa Bodi walipwe Shilingi 4,800,000 kwa kila mjumbe kwa mwaka 2022. | Malipo ya wakurugenzi kwa mwaka 2022, yalilipwa kiasi cha kiasi cha shilingi 4,800,000. |
| **17.11** | Kampuni kununua Baadhi ya hisa zake (Share buy Back) | Kampuni itenge kiasi cha Shs milioni 100 kwa ajili ya kununua hisa zake. | Suala hili limekataliwa na soko la mtaji kwa kuwa halikubaliki kisheria hata hivyo Bodi itawasilisha jambo hili kwa mamlaka nyingine kwa ushauri hata hivyo hisa za wanahisa wadogo ambazo zilikuwa hazijanunuliwa zimepata mnunuzi. |
| **17.12** | Pendekezo la kuorodhesha hisa za kampuni kwenye soko la hisa la afrinex- mauritius (cross-listing) | Kampuni iliorodhesha hisa zake kwenye soko la hisa la AFRINEX MAURITIUS. | Liko katika hatua ya utekelezaji mara tu baada ya kubadilisha jina la kampuni. |



# KUPOKEA, KUJADILI NA KURIDHIA TAARIFA YA WAKURUGENZI WA BODI YA KAMPUNI NA TAARIFA YA MAHESABU YALIYOKAGULIWA KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 31 DESEMBA, 202.



Taarifa ya Mahesabu yaliyokaguliwa iko katika Taarifa ya Mwaka.

## TAARIFA YA MWENYEKITI

*"Tunahitaji kuhakikisha Kampuni inakua pamoja na kuimarisha mifumo ya utendaji na kuwa na biashara endelevu. Hatua kwa hatua, tunaweza kugeuza maono ya kampuni na kutengezeza faida zaidi kwa wanahisa."*

*Fortunatus M. Magambo*



**TAARIFA YA MWENYEKITI**

**UTANGULIZI**

Bodi ya Wakurugenzi inayo furaha kuwasilisha Taarifa yake pamoja na Taarifa ya Mahesabu kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Desemba 2022. Kama kawaida, kwa mwaka wa fedha, 2022 Kampuni yetu ilipata mafanikio makubwa. Katika ulimwengu wenye ushindani mkubwa wa kibiashara, Bodi imechukua hatua madhubuti za kuimarisha hali ya kifedha ya Kampuni ili wanahisa wapate faida ya kile walichopanda kwa jasho wakati huu ambao upanuzi wa wigo wa uwekezaji unapofanyika.

**BIASHARA ENDELEVU**

Biashara endelevu inabakia kuwa kipengele muhimu katika kuboresha ukuaji wa uchumi wa Kampuni. Tuna imani na uwezo wa kuhakikisha kuwa Kampuni inaendelea kufanya vizuri katika utendaji katika kufikia malengo iliyojiwekea ili kuunda Kampuni thabiti. Tayari, biashara endelevu imekuwa ni sehemu muhimu ya shughuli zetu. Ni utaratibu muhimu katika kushirikiana na washikadau wetu ili kutoa suluhisho bora, salama kwa kuzingatia mazingira ya sasa.

Lengo letu ni kuharakisha ukuaji wa Kampuni unaotokana na uvumbuzi, kuimarisha ushirikiano, na kukamilisha maendeleo ya jumla na endelevu. Kidogo kidogo, tuna uhakika wa kutambua maono yetu na kukidhi matakwa ya wanahisa wetu.

**GAWIO**

Bodi ya Wakurugenzi inapendekeza gawio la Shilingi 13 kwa kila hisa moja kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Desemba 2022 (2021: Shilingi10). Malipo ya gawio yanategemewa kuidhinishwa na wanahisa wakati wa Mkutano Mkuu wa Mwaka.

**MATARAJIO YA BAADAYE**

Kwa kuzingatia msukumo wa kuifanya Kampuni kuwa yenye mafanikio, Bodi itaendelea kufanya kazi kwa bidii ili kuongeza njia za mapato na kuboresha ufanisi wa kazi; lengo ikiwa ni kupata fursa mpya kitaifa na kimataifa.

**SHUKRANI**

Natoa shukrani zangu kwa wajumbe wenzangu wa Bodi ya Wakurugenzi na wafanyakazi ambao kupitia wao nimeweza kupanua uwezo wangu wa kufikiri na kupanua Kampuni yetu hadi ngazi za kitaifa na kimataifa. Ninawashukuru wanahisa wetu, wadau, na washirika wetu wa kibiashara kwa msaada wao ili kuhakikisha Kampuni inastawi. Wala siwezi kusahau jukumu kubwa linalofanywa na CMSA (Mamlaka ya Soko la Mitaji na Dhamana), DSE (Soko la Hisa la Dar es Salaam) na vyombo vingine vya udhibiti kwa usaidizi wao usio na kifani.

Mwisho, Menejimenti kwa kujitolea katika usimamizi wa maono mapana ya Kampuni na kuwa bora kuelekea katika ustawi.

Ahsante Sana,

..............................................

**Fortunatus Makore Magambo,**
Mwenyekiti wa Bodi

## TAARIFA YA AFISA MTENDAJI MKUU

*"Kampuni imedumisha ukuaji thabiti na ongezeko la mapato pamoja na uwekezaji. Taarifa ya utendaji pamoja na fedha kwa mwaka 2022 ukilinganisha na taarifa ya mwaka 2021 imeainishwa kwenye jedwali hapa chini: "*

Peter W. Kifunguomali



### UTANGULIZI

Kwa mwaka huu wa tatu wa utekelezaji wa Mpango Mkakati wa mwaka 2020-2022, Kampuni imepiga hatua kubwa mbele kwani mafanikio makubwa yameonekana kufikia tarehe 31 Desemba 2022.
Kuridhika kwa wanahisa, kupata faida, uhakika katika mtiririko kifedha na ukuaji wa mapato, ni malengo muhimu yaliyomo katika mpango wa miaka mitatu ambao lengo lake ni kubadilisha mienendo ya sasa na ya baadaye huku Kampuni ikiendelea kukua ili kufanya vizuri kitaifa na kimataifa. Kimsingi, Mpango Mkakati unazingatia mambo muhimu kama vile ongezeko la thamani kwa Wanahisa, Uwekezaji na Ubora wa Utendaji. Menejimenti na Bodi ya Wakurugenzi wanafanya kazi kwa bidii ili kuhakikisha kuwa Kampuni inafanikiwa kufikia malengo yaliyowekwa. Kuna mwanga unaonenyesha matarajio mazuri ya Kampuni kwa siku za mbele.

### TAARIFA YA KIUTENDAJI

Kampuni imedumisha ukuaji thabiti na ongezeko la mapato pamoja na uwekezaji. Taarifa ya utendaji pamoja na fedha kwa mwaka 2022 ukilinganisha na taarifa ya mwaka 2021 imeainishwa kwenye jedwali hapa chini:

### UCHAMBUZI KATIKA UWEKEZAJI

Kwa 2022, mpango mkakati wa Kampuni katika uwekezaji uliingia katika mwaka wake wa tatu wa utekelezaji.

*Jedwali na. 2*

| MAELEZO | MAELEZO | 2021 | 2022 |
|---|---|---|---|
| Mapato | Shilingi'000 | 2,690,726 | 2,997,973 |
| Gharama za Uendeshaji wa Kampuni | Shilingi'000 | 1,014,149 | 1,072,564 |
| Faida baada ya Kukata Kodi | Shilingi'000 | 1,329,859 | 1,959,810 |
| Mtaji wa Wanahisa | Shilingi'000 | 27,404,314 | 32,329,051 |
| Jumla ya mali za Kampuni | Shilingi'000 | 30,451,345 | 35,216,671 |
| Mapato kwa kila hisa | Shilingi'000 | 18.67 | 27 |

Kwa ujumla, malengo yaliyopangwa na Kampuni yalifikiwa kwa kiasi kikubwa. Rasilimali halisi za Kampuni ziliongezeka kwa asilimia 18 ikilinganishwa na thamani ya Shilingi 27 bilioni mwezi Desemba, 2021. Kwa ujumla, malengo yaliyopangwa ya Kampuni yalifikiwa kwa kiasi kikubwa. Kampuni ina mali zenye thamani ya Shilingi 35 bilioni, ambapo Shilingi 34 bilioni ipo katika uwekezaji. Uwekezaji uliongezeka kwa asilimia 15 ikilinganishwa na thamani ya Shilingi 29 bilioni mwezi Desemba, 2021.

*Jedwali na. 3*

| AINA YA UWEKEZAJI | 2021 (SHS'000') | % | 2022 (SHS'000') | % |
|---|---|---|---|---|
| Amana za Serikali | 12,985,104 | 44 | 13,589,143 | 40 |
| Hisa Zilizoorodheshwa | 15,253,840 | 52 | 19,620,534 | 58 |
| Fedha Taslimu | 932,472 | 3 | 335,000 | 1 |
| Mali za Kampuni | 221,347 | 1 | 221,347 | 1 |
| Amana za Makampuni | – | – | 150,000 | – |
| Jumla ya Uwekezaji | 29,392,763 | 100 | 33,916,024 | 100 |

**MTAZAMO WA BIASHARA**


Kuanzisha miradi katika maeneo muhimu kama vile kilimo na biashara ya mifugo inayowagusa Watanzania walio wengi ndiyo lengo letu kubwa kwa kuzingatia mazingira mazuri ya uwekezaji yaliyopo. Kujihusisha katika maeneo ya uzalishaji kutaleta manufaa tunapothamini mienendo ya uchumi wa nchi.

Hata hivyo, tutategemea pia kupunguza uwekezaji kwenye hisa ili kupunguza uwezekano wa athari zinazoweza kujitokeza na kuathiri mwenendo wa Kampuni.

**HITIMISHO**

Tuna wafanyakazi bora na waliojitolea kuwa familia ya TCCIA Investment PLC wenye bidii na wanaofahamu vyema maadili ya Kampuni kwa utendaji bora. Ninaishukuru Bodi ya Wakurugenzi kwa mwongozo mzuri, Menejimenti kwa kufanya kazi kwa pamoja, mabenki, Wakaguzi wa Mahesabu, na wawekezaji kwa kujitolea kwao kuhakikisha Kampuni inastawi katika hali ya ushindani mkali wa kibiashara.

Ahsanteni sana



......................................

**Peter William Kifunguomali**
Afisa Mtendaji Mkuu
Tarehe: **27/05/2023**

# TAARIFA YA WAKURUGENZI KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 31 DESEMBA, 2022

## UTANGULIZI

Bodi ya Wakurugenzi inayo furaha kuwasilisha Taarifa ya Wakurugenzi pamoja na Taarifa ya Mahesabu yaliyokaguliwa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Desemba, 2022. Taarifa hii inatoa picha kamili ya hali halisi ya Kampuni kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 31 Desemba, 2022.

## UANZISHWAJI WA KAMPUNI

Kampuni ilianzishwa Tanzania kulingana na Sheria za Makampuni ya mwaka 2002. Kampuni imesajiliwa na Soko la Hisa la Dar es Salaam na inamilikiwa na wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## BIASHARA YA KAMPUNI

Biashara kuu ya Kampuni ni uwekezaji katika hisa za Makampuni yaliyoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam ikiwa ni pamoja na Amana za Makampuni ambazo zinatoa faida kubwa na Amana za Serikali pamoja na uwekezaji katika maghala ambayo yako maeneo yenye mpango mkakati mzuri.

Aidha, Kampuni inahimiza kujenga utamaduni wa kuweka akiba kwa wanahisa wake kwa njia ya kuwekeza katika hisa za makampuni yenye ufanisi mkubwa.

## MAONO, DHIMA, KAULI MBIU NA MAADILI KATIKA KAZI

**DHIMA YA KAMPUNI**
Kutengeneza ongezeko la thamani ya muda mrefu kwa wanahisa wa Kampuni kwa kutoa faida nzuri zaidi inayotokana na uwekezaji bora na salama.

**MAONO YA KAMPUNI**
Kuwa kituo kikuu cha usimamizi wa uwekezaji Tanzania.

**KAULI MBIU**
Kwa pamoja tunaweza.

**MAADILI KATIKA KAZI:**
Uwajibikaji, Kujitoa, Kufanya kazi kwa pamoja, Uaminifu na uvumbuzi.

## MATOKEO YA SHUGHULI ZA BIASHARA

Taarifa za Mahesabu zinaandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya uandaaji wa Taarifa za Mahesabu (IFRS) na Sheria ya Makampuni ya mwaka 2002. Sera za uhasibu zimetumika ipasavyo ikilinganishwa na mwaka jana.

Kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Desemba, 2022, Kampuni ilipata faida ya Shilingi 1,959,810,000 baada ya kodi ikilinganishwa na Shilingi 1,329,859,000 mwaka 2021 baada ya kodi. Mapato ya Kampuni yaliongezeka kwa asilimia saba (11%) kutoka Shilingi 2,690,726,000 mwaka 2021 na kufikia Shilingi 2,997,973,000 mwaka 2022. Kuongezeka kwa mapato kunatokana na uamuzi wa Bodi wa kubadilisha mfumo wa uwekezaji wa Kampuni na kuwekeza zaidi katika Amana za Serikali na kwenye hisa.

## IDADI YA HISA ZA KAMPUNI

*Jedwali na. 4*

| | | | IDADI YA HISA 2022 | 2021 |
|---|---|---|---|---|
| Zilizoidhinishwa (Authorized) | | | | |
| Hisa za Kawaida (Ordinary Shares) | | | 5,000,000,000 | 5,000,000,000 |
| | | | | |
| | 2022 | 2021 | 2022 | 2021 |
| | Shs'000 | Shs'000 | Idadi ya Hisa | |
| Hisa za Kawaida (Ordinary Shares) | 1,459,153 | 1,459,153 | 72,957,660 | 72,957,660 |
| Share Premium | 708,799 | 708,799 | - | - |
| | 2,167,952 | 2,167,952 | 72,957,660 | 72,957,660 |

Hapakuwa na mabadiliko yoyote ya idadi ya hisa zinazomilikiwa na Kampuni kwa mwaka 2021.

## GAWIO

Kwa mwaka wa fedha ulioishia Desemba 31, 2022, Bodi inapendekeza gawio la Shilingi 13 kwa kila hisa moja ambayo ni sawa na Shilingi 948,449,580 ukilinganisha na gawio la Shilingi 10 kwa kila hisa moja sawa na Shilingi 729,576,600 mwaka 2021.

## DHUMUNI NA MPANGO MKAKATI WA KAMPUNI

**Ongezeko la Thamani**: Kuiwezesha Kampuni kufikia lengo la wanahisa la kuanzishwa kwa hii Kampuni. Lengo kuu ni kuongeza thamani ya Hisa na kukuza mtaji wa Kampuni. Kampuni pia inalenga kuanzisha Kampuni tanzu ili kugawanya mtaji wake katika maeneo mengine ya biashara.

**Uwekezaji Bora:** Kampuni ina lengo la kuimarisha thamani ya Kampuni kwa kuimarisha rasilimali za Kampuni na kuongeza kipato katika uwekezaji. Kampuni ina mpango wa kukuza kipato kupitia uwekezaji kwa asilimia kumi na mbili (12%) kwa mwaka.

**Utendaji Bora:** Kampuni ina mpango wa kuimarisha utendaji kupitia wafanyakazi waliopo na teknolojia ili kukuza ufanisi, kuhudumia wanahisa, kukidhi matakwa ya mamlaka zinazoisimamia, kuimarisha utamaduni wa ushirikiano, kuimarisha maslahi ya wafanyakazi na kuimarisha utendaji na uwajibikaji wa wafanyakazi. Pia, Kampuni ina mpango wa kufanikisha mipango yake kwa asilimia tisini na tano (95%).

## WAKURUGENZI WA KAMPUNI

Kwa mwaka wa Fedha ulioishia Desemba 31, 2022, Wakurugenzi walikuwa ni hawa wafuatao:-

*Jedwali na. 5*

| JINA | NAFASI | URAIA | SIFA/ELIMU |
|---|---|---|---|
| Bw. Fortunatus Magambo | Mwenyekiti | Mtanzania | Mchumi |
| Prof. Lucian A. Msambichaka | Makamu Mwenyekiti | Mtanzania | Mchumi |
| Bw. Joseph M. Kahungwa | Mjumbe | Mtanzania | Mhasibu |
| Bi. Magdalene N. E. Mkocha | Mjumbe | Mtanzania | Kilimo/Mchumi |
| Bw. Nathan E. Mnyawami | Mjumbe | Mtanzania | Mchumi |
| Bw. Ernest R. Khisombi | Mjumbe | Mtanzania | Mauzo na Manunuzi |
| Bw. Paul F. Koyi | Mjumbe | Mtanzania | Teknohama |

Hapakuwa na mabadiliko yoyote ya Wakurugenzi kwa mwaka 2022.

## MATUKIO BAADA YA TAARIFA HII

Hapakuwa na tukio lolote lililojitokeza baada ya kutolewa kwa taarifa hii.

## KATIBU WA BODI

Kwa mwaka ulioishia Desemba 31, 2022, hapakuwa na mabadiliko yoyote ya Katibu, bali ameendelea kuwa Ndugu Peter William Kifunguomali.

## SIASA NA KUSAIDIA JAMII

Kulingana na Sera ya Kampuni, hatujawahi kuchangia shughuli za kijamii. Hivyo kwa mwaka 2022 hakuna mchango wowote uliotolewa.

## UDHIBITI WA ATHARI ZINAZOWEZA KUJITOKEZA NA MFUMO WA NDANI

Bodi ina wajibu wa kudhibiti athari zinazoweza kujitokeza pamoja na kusimamia mfumo mzima wa utendaji kwenye Kampuni. Menejimenti inawajibika kuhakikisha taarifa ya Mahesabu na Mfumo wa Utendaji unafanya vizuri. Lengo ni kuhakikisha ufanisi katika mfumo wa utendaji kama ifuatavyo:

- Kulinda stahiki za wanahisa na mali za Kampuni.
- Ufanisi na Ubora katika kazi;
- Kukidhi matakwa ya Mamlaka na Sheria.
- Kuwepo kwa rekodi ya Mahesabu na Taarifa ya Fedha.
- Kampuni kuendelea na shughuli za utendaji katika mazingira ya kawaida na yasiyo ya kawaida.
- Kuwajibika kwa wadau wa Kampuni.

Ufanisi na udhibiti wa mfumo wowote wa utendaji wa ndani unategemea utaratibu na hatua zilizochukuliwa. Kuna athari zinazoweza kujitokeza kwa kushindwa kufuata taratibu zilizowekwa kwa wafanyakazi. Hakuna mfumo wa udhibiti wa ndani unaoweza kutoa taarifa kamili dhidi ya taarifa potofu au hasara kwa sababu mfumo wa Kampuni umeundwa kuwapa Wakurugenzi uhakika kwamba taratibu zilizopo zinafanya kazi kwa ufanisi. Wakurugenzi wamethibitisha mfumo wa ndani wa utendaji na kujiridhisha kuwa unafanya kazi vizuri.

Kampuni ina sera mbalimbali ambapo kupitia hizo inaweza kudhibiti athari kwenye Kampuni. Na kwa upande mwingine, Kampuni imemwajiri Mkaguzi wa ndani wa muda, ambaye anasimamiwa na Bodi kupitia Kamati ya Ukaguzi ambapo kupitia yeye Bodi inaweza kusimamia utendaji wa Kampuni kwa ufanisi mkubwa.

### Tathmini na Athari za Kampuni na Namna ya Kuzizuia.

Kampuni imewekeza katika taasisi za fedha ikiwemo Amana za serikali za muda mfupi na muda mrefu, Amana za Makampuni, mikopo, amana za mabenki na kwenye hisa. Maeneo mengine ya uwekezaji ni pamoja na biashara zinazotoa faida. Lengo la uwekezaji huu ni kuongeza mapato kwenye Kampuni.

Athari zinazoweza kuikumba Kampuni ni pamoja na: -

### Athari za Kutopata Faida

Athari ya kutopata faida ni athari ya soko inayotokana na mabadiliko ya thamani ya mali ya Kampuni kama matokeo ya kushuka kwa bei katika uwekezaji wa Kampuni. Uwekezaji katika amana za serikali za muda mrefu na mapato ya kudumu ni njia mojawapo ya kupunguza athari ya kushuka kwa viwango vya riba katika soko.

### Athari ya Hisa Kushindwa Kuuzwa

Hii athari inatokana na kushindwa kufikia malengo. Lakini pia hii athari inatokana na kushindwa kuuza hisa kwa wakati na kwa bei iliyokusudiwa. Kampuni inaweza kupunguza hii athari kwa kuwekeza kwenye amana za benki za muda mfupi zinazoweza kukamilisha mipango yake ya uwekezaji na matumizi ya ndani ya Kampuni.

Kampuni imekuwa ikifanya makisio ya mapato na matumizi ya kila mwezi. Kampuni inategemea kipato chake kikubwa toka kwenye Magawio kutoka kwenye Makampuni inayomiliki hisa na maeneo mengine ilikowekeza.

**Athari za Mikopo**

Hii inatokana na upande mmoja kushindwa kutimiza wajibu wake wa kulipa deni kwa tarehe iliyopangwa. Ili kupunguza hii athari, Kampuni imeandaa sera ya uwekezaji, kutathmini kabla ya kufanya uwekezaji na ngazi za uidhinishaji katika kila eneo la uwekezaji.

**Athari za Kiutendaji**

Hii inatokana na mfumo duni, usimamizi dhaifu, utendaji dhaifu, udanganyifu katika kazi, wizi na makosa mengine ya kibinadamu. Kampuni inajitahidi kuiepuka hii athari kwa kuweka mfumo mzuri wa usimamizi wa ndani wa Kampuni. Moja ya mbinu za kudhibiti ni pamoja na kufuata miongozo ya kiutendaji na taratibu zilizowekwa, sera na miongozo na kuajiri Mkaguzi wa ndani wa muda. Kusimamia athari za kiutendaji katika Kampuni ni muhimu katika shughuli za kila siku. Kamati ya usimamizi, Mkaguzi wa Ndani wa muda, Kamati ya Ukaguzi na Bodi ya Wakurugenzi wanahusika kikamilifu katika usimamizi wa Kampuni.

**Athari za Rasilimali Watu**

Kulingana na uhalisia wa shughuli za Kampuni, inahitaji wafanyakazi wenye nidhamu na wenye maarifa maalum katika maeneo muhimu ya kiutendaji. Muundo wa Wafanyakazi wa Kampuni unaisaidia Kampuni kuingiza mapato makubwa. Ili kuhakikisha athari hii ya rasilimali watu inazuiwa, Kampuni inahakikisha inawekeza kwa wafanyakazi wake, kupitia kuboresha maslahi yao kila mara.

**Athari ya Kampuni Kupoteza Sifa yake Nzuri**

Kampuni ina wajibu wa kuhakikisha majukumu yake yanafanyika vizuri ili kulinda sifa yake katika makampuni yaliyoorodheshwa kwenye Soko la Hisa kulingana na sheria na taratibu husika. Katika kuhakikisha hili linafanyika, Bodi na Menejimenti zinahakikisha zinatimiza wajibu wake kwa kuzingatia sheria za utawala bora.

**Idadi ya Hisa zinazomilikiwa na Wajumbe wa Bodi kwenye Kampuni**

Mpaka kufikia Desemba 31, 2022, idadi ya Hisa za kila Mjumbe wa Bodi ni kama ifuatavyo:

*Jedwali na. 6*

| WAKURUGENZI | IDADI YA HISA ANAZOMILIKI | |
|---|---|---|
| | 2022 | 2021 |
| Prof. Lucian Ambrose Msambichaka | 65,880 | 487,580 |
| Bw. Joseph Matanga Kahungwa | 40,600 | 40,600 |
| Bw.Nathan Edward Mnyawami | 19,675 | 19,675 |
| Bi. Magdalene Nelson Enock Mkocha | 102,363 | 102,363 |
| | **229,918** | **650,218** |

- Bw. Paul F. Koyi, Rais wa TCCIA - Anawakilisha TCCIA Makao Makuu na Ofisi za Matawi yake zilizoko Mikoa yote ya Tanzania ambao wanamiliki jumla ya Hisa 830,213.
- Bw. Fortunatus Magambo and Bw. Ernest R. Khisombi kwa pamoja wanawakilisha Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Serikali (PSSSF) unaomiliki jumla ya Hisa 28,100,300.


Hakuna mabadiliko yaliyojitokeza kati ya kipindi cha uandaaji wa taarifa hii hadi leo inapowasilishwa.

**UTAWALA BORA**

Bodi inawajibika kwa shughuli zote za Kampuni. Pamoja na mambo mengine, Bodi ina wajibu wa kutambua athari ambazo zinaweza kuathiri shughuli za Kampuni, kutafuta fursa na kufanya maamuzi yahusuyo uwekezaji. Bodi ina wajibu wa kuhakikisha mfumo wa utendaji unadhibitiwa ipatasavyo pamoja na sera zote zinatumika na mfumo wa Utawala bora unafuatwa pamoja na taratibu zote.

Kwa mwaka wa fedha ulioishia Desemba 31, 2022, Bodi ilikutana mara nane (8), ambapo Vikao vya kawaida vilikuwa nne (4) na vikao maalum vinne (4) ambavyo vilifanyika kuidhinisha mambo muhimu ambayo yalikuwa yanahitaji idhini ya Bodi. Bodi imekabidhi usimamizi wa shughuli za kila siku za Kampuni kwa Afisa Mtendaji Mkuu akisaidiwa na Menejimenti. Menejimenti pia inaalikwa kuhudhuria vikao vya Bodi ili kuimarisha ufanisi katika shughuli za Kampuni na Utawala bora. Lengo la kufanyika kwa vikao maalum, ni pamoja ya kujadili na kuidhinisha Mpango Mkakati wa Kampuni na Bajeti ya mwaka pamoja na kupitia Taarifa ya Mahesabu yaliyokaguliwa.

**WAJUMBE WA BODI PAMOJA NA IDADI YA VIKAO WALIVYOHUDHURIA KWA MWAKA 2022.**




*Jedwali na. 7*

| NA. | JINA | NAFASI | IDADI YA VIKAO | IDADI YA VIKAO ALIVYOHUDHURIA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Bw. Fortunatus Magambo | Mwenyekiti | 8 | 8 |
| 2. | Prof. Lucian A. Msambichaka | Makamu Mwenyekiti | 8 | 8 |
| 3. | Bw. Joseph M. Kahungwa | Mjumbe | 8 | 8 |
| 4. | Bi. Magdalene N. E. Mkocha | Mjumbe | 8 | 8 |
| 5. | Bw. Nathan E. Mnyawami | Mjumbe | 8 | 8 |
| 7. | Bw. Paul F. Koyi | Mjumbe | 8 | 7 |
| 8. | Bw. Ernest R. Khisombi | Mjumbe | 8 | 8 |

Wakurugenzi wote wana sifa na uzoefu unaojitegemea ambao unasaidia katika kufanya maamuzi. Wakurugenzi wote wana tabia njema na wanatekeleza majukumu yao kwa uadilifu.

Wakurugenzi wote wanafuata kanuni za Utawala Bora. Kwa mwaka wa fedha wa 2022, Bodi iliunda Kamati mbili ili kutimiza kanuni za Utawala Bora na kufanya maamuzi kwa wakati sahihi kuhusiana na mambo ya Kampuni. Kamati hizo ni:-

- Kamati ya Uwekezaji ambayo ina wajumbe watatu.
- Kamati ya Ukaguzi na Kuzuia Athari katika Kampuni ambayo ina wajumbe watatu.

*Jedwali na. 8*

| | Wajumbe wa Kamati ya Uwekezaji: | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Prof. Lucian A. Msambichaka | Mwenyekiti | |
| 2. | Bw. Nathan E. Mnyawami | Mjumbe | |
| 3. | Bw. Paul F. Koyi | Mjumbe | |

Kamati ya Uwekezaji ilikutana mara nne (4) kujadili taarifa ya Kampuni ya kila robo mwaka, na Mpango Mkakati wa mwaka pamoja na Bajeti ya Kampuni kabla ya kuwasilisha kwenye Bodi kwa majadiliano na kuidhinisha.

### WAJUMBE WA KAMATI YA UKAGUZI NA KUZUIA ATHARI KATIKA KAMPUNI: -

*Jedwali na. 9*

| | WAJUMBE WA KAMATI YA UKAGUZI NA KUZUIA ATHARI KATIKA KAMPUNI: | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Bw. Joseph M. Kahungwa | Mwenyekiti | |
| 2. | Bw. Ernest R. Khisombi | Mjumbe | |
| 3. | Bi. Magdalene N. E. Mkocha | Mjumbe | |

Kamati ya Ukaguzi na Kuzuia Athari katika Kampuni ilikutana mara sita (6) kujadili Taarifa ya Kampuni inayoandaliwa na Mkaguzi wa ndani na pia kupitia mahesabu ya Kampuni ya Mwaka mzima.

### MAJUKUMU YA BODI KWA MWAKA 2022

Pamoja na Kusimamia shughuli za Bodi kwa mwaka 2022, Bodi ina majukumu yafuatayo:-

- Kuhakiki Taarifa za wanahisa wa Kampuni;
- Kupitia taarifa ya Kampuni iliyoandaliwa na Mkaguzi wa ndani;
- Kutafuta njia mbalimbali za kupunguza gharama za uendeshaji wa Kampuni na kuongeza mapato;
- Kuandaa mpango mkakati na kupitisha bajeti ya mwaka 2023;
- Kufanya Upembuzi yakinifu na kutafuta vyanzo vipya vya uwekezaji.

### KUKIDHI MATAKWA YA KISHERIA

Kampuni imeendelea kuwa na uhusiano mzuri na wadau wake. Lakini pia Kampuni imeendelea kuwa na uhusiano mzuri na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Usimamizi wa Mitaji na Dhamana (CMSA), Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE), Madalali wa Soko la Hisa (Brokers) na benki za Biashara. Kwa mwaka 2022, Kampuni imeweza kutimiza taratibu na vigezo vyote kulingana na Matakwa ya Mamlaka husika.

### UPATIKANAJI WA TAARIFA YA MAHESABU

Kampuni ina wafanyakazi wenye uzoefu katika kitengo cha uhasibu na fedha. Vitabu vya mahesabu vimekuwa vikitunzwa na taarifa ya fedha inaandaliwa kulingana na Sheria ya Kimataifa ya Uandaaji wa taarifa za Mahesabu. (IFRS).

### MTAJI WA KAMPUNI

Mtaji wa Kampuni ulioidhinishwa ni Shilingi 100,000,000,000 ambapo umegawanywa katika mfumo wa hisa, ambapo kufikia Desemba 31, 2022 thamani ya hisa moja ilikuwa sawa na Shilingi 20. Hisa zilizokuwa zimelipiwa ni sawa na Shilingi 2,167,952.000

*Jedwali na. 10*

| | 2022<br>Shs'000 | 2021<br>Shs'000 |
|---|---|---|
| Mtaji wa Kampuni Ulioidhinishwa (Shs)<br>5,000,000,000 hisa za kawaida zenye thamani ya Shilingi 20 kwa hisa moja. | 100,000,000 | 100,000,000 |
| **Hiza zilizolipiwa**<br>72,957,660 hisa za kawaida zenye thamani ya Shilingi 20 kwa kila hisa. | 1,459,153 | 1,459,153 |
| Share Premium | 708,799 | 708,799 |
| | 2,167,952 | 2,167,952 |

**MTAJI WA KAMPUNI NA UMILIKI WAKE.**

*Jedwali na. 11*

| UMILIKI WA HISA | ASILIMIA | SHS'000 |
|---|---|---|
| PSSSF | 39 | 562,006 |
| | | |
| Abbasi Export Ltd | 10 | 144,591 |
| Christopher Mwita Gachuma | 2 | 29,591 |
| Fayaz Feroz Rashid | 2 | 24,728 |
| Nimrod Elirehemah Mkono | 2 | 22,480 |
| Wanahisa wengine (less than 1.5) | 45 | 676,143 |
| | 100 | 1,459,153 |

## TAARIFA KUHUSU SOKO LA HISA

Kampuni imeorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam. Mpaka kufikia Desemba 31, 2022, thamani ya hisa moja ilikuwa Shilingi 155 ambayo ni sawa na thamani ya hisa moja  na mtaji wa Soko ulikuwa Shilingi 11,336,000,000 ambayo ni sawa na mtaji wa mwaka 2022. Disemba 2021 Shs 350 mtaji Shs 25,580,000,000.

## BIASHARA ENDELEVU

Katika majadiliano ya Bodi katika kuimarisha ukuaji wa Kampuni, haukuzingatia kushuka na kupanda kwa thamani ya fedha. Bodi ilizingatia kulinda na kuhakikisha Kampuni inaendeleza utendaji wake, mabadiliko ya tabia nchi na rasilimali zinazohitajika ili Kampuni iendelee kufanikiwa kwa miaka ijayo. Lakini pia tunaamini katika kuimarisha mazingira ya utendaji katika kuepuka kuwekeza kwenye miradi ambayo itaharibu sifa nzuri ya Kampuni hata kama utakuwa na faida kubwa; kuhimiza wafanyakazi na wadau wa Kampuni kujiendeleza, kujizoeza na kutumia teknolojia, kutumia mtandao, kuongeza upeo wa wafanyakazi wa TICL katika utendaji na kuwahimiza wadau wa Kampuni kuhusu kuondoa madhara ya kimfumo kupitia teknolojia. Kuelimisha kuhusu programu ya uhamasishaji wa teknolojia rafiki kwa mazingira (Corporate Social Responsibilities).

## MTAZAMO KATIKA KUENDELEA KWA SHUGHULI ZA KAMPUNI

Wakurugenzi wanaamini kuwa, Kampuni ina rasilimali za kutosha za kifedha kuendelea kufanya kazi kwa siku zijazo kulingana na Taarifa ya Mahesabu iliyoambatanishwa. Wakurugenzi wamejiridhisha kuwa, Kampuni iko katika hali nzuri ya kifedha na kwamba ina uwezo wa kukopa ili kukidhi mahitaji yake ya kifedha pale itakapohitajika. Wakurugenzi hawajapokea taarifa mpya ambayo inaweza kuathiri utendaji wa Kampuni hapo baadaye.

## MASLAHI YA WAFANYAKAZI

Kampuni inawapa wafanyakazi wake maslahi yafuatayo:

### Elimu

Kampuni inawafadhili wafanyakazi wake kujiendeleza kielimu katika kozi za muda mfupi ndani na nje ya nchi kwa taaluma mbalimbali kulingana na uhitaji na kiwango cha fedha kinachohitajika. Kampuni pia inasaidia wafanyakazi pale wanapoamua kujiendeleza wenyewe kwa masomo ya muda mrefu.

### Mikopo kwa Wafanyakazi

Kampuni inatoa mikopo kwa wafanyakazi ya muda mrefu na mfupi kuweza kutatua matatizo ya kifedha na kufanya shughuli nyingine za kiuchumi za kujiongezea kipato. Mikopo hiyo inatolewa kulingana na masharti yaliyowekwa na Bodi na inatolewa kulingana na Bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka husika.

### Msaada wa Kifedha

Kampuni inaandaa sera ya kusaidia pale mfanyakazi anapofariki au wategemezi.

### Mafao ya Kustaafu

Kampuni inachangia kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ikiwemo Public Servant Social Security Fund (PSSSF) na National Social Security Fund (NSSF) kwa ajili ya mafao ya baadaye kwa wafanyakazi wake.

### Watu wasiojiweza (Walemavu wa Viungo)

Kampuni inatoa nafasi sawa ya ajira kwa watu wote yaani wenye viungo vyote na wale wenye ulemavu wa viungo.

### Huduma ya Matibabu

Kampuni imeingia mkataba na Shirika la Bima ya Afya la Taifa (NHIF) kutoa huduma ya afya kwa wafanyakazi wa Kampuni na wategemezi wao.

### Usawa wa Kijinsia Kazini

Kufikia Desemba 31, 2022, Kampuni ilikuwa na wafanyakazi 6 sawa na mwaka 2021. Wafanyakazi watatu wakiwa ni wanawake na watatu wanaume.

### Mazingira, Jamii na Utawala

Tunaendelea kuzingatia masuala ya Mazingira, Kijamii na Utawala na tumetambua njia bora zaidi za kupima kile ambacho tumekuwa tukikifanya. Kampuni imejitolea "kuwa kijani" kwa kufanya kazi bila kutumia karatasi na kutenga uwekezaji wetu wa hisa katika makampuni ambayo yanatii sheria za mazingira na usalama.

## MIPANGO YA BAADAYE YA MAENDELEO

Kuanzia mwaka 2018, Bodi ya Wakurugenzi iliamua kupunguza uwekezaji wake kwenye hisa na kuwekeza maeneo mengine ambayo ilikuwa bado haijawekeza. Toka Kampuni imeanza kufanya shughuli za biashara Oktoba, 2005 zaidi ya asilimia tisini na tano (95%) ya uwekezaji wake ilikuwa ni kwenye hisa za makampuni yaliyoorodhesha  hisa zake

kwenye Soko la Hisa. Bodi iliamua kuwekeza kwenye maeneo yenye mapato ya uhakika (Amana za Serikali, Amana za Makampuni na faida inayotokana na Amana za Mabenki). Bodi ya Wakurugenzi inaamini kwa kuwekeza katika taasisi hizi za kifedha ni biashara nzuri kwa kuzingatia pale ambapo Soko la Hisa litashindwa kufanya vizuri kama ilivyo sasa ambapo kipato chake hakitabiriki.

Bodi ya Wakurugenzi imeamua kuelekeza uwekezaji wake kwenye amana za serikali kwa sababu faida yake ni ya uhakika ukilinganisha na uwekezaji katika hisa.

Mwisho, Bodi inapenda kuainisha maeneo mengine ya uwekezaji kama kuagiza na kuuza bidhaa nje ya nchi, biashara ya mifugo, na biashara nyingine katika sekta ya fedha kama kuuza na kununua Amana za Makampuni na Serikali.

**Kulinda Mali za Kampuni**

Wakurugenzi wana jukumu la kulinda mali za Kampuni. Bodi imeidhinisha sera mbalimbali na kanuni ambazo hazikinzani na Mamlaka za fedha, na sera ya uwekezaji ili kuimarisha mazingira ya udhibiti wa mfumo wa ndani. Sera hizi hupitiwa mara kwa mara ili kuenenda na mazingira ya sasa ya utendaji. Wakurugenzi wanayo furaha kutoa taarifa kwamba kwa mwaka 2022 hapakuwa na matukio yoyote ya udanganyifu.

**Mambo yahusuyo Miamala**

Mambo yote yahusuyo miamala na kiwango cha fedha kilichopo kimeonyeshwa katika kifungu cha 32 cha Taarifa ya Fedha.

**Wajibu wa Wakurugenzi**

Ni wajibu wa Wakurugenzi kuhakikisha kwamba taarifa za fedha zinawasilishwa kwa kila mwisho wa mwaka wa fedha na matokeo ya shughuli za utendaji kwa kipindi kilichomalizika, kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa taarifa za Fedha na taratibu zinazotumika, kanuni na matakwa ya kisheria. Wakurugenzi pia wanathibitisha matakwa ya Uandaaji wa Taarifa za Fedha Tanzania (TFRS 1) na sheria zingine zote zinazohusiana na Kampuni.

**WAKAGUZI WA MAHESABU YA KAMPUNI**

Wakaguzi wa Mahesabu, Crowe Tanzania, wameendelea kuonyesha nia yao ya kuendelea kukagua mahesabu ya Kampuni endapo watateuliwa tena, kwa mwaka wa fedha utakaoishia tarehe 31 Desemba 2023. Hata hivyo, Bodi itawasilisha pendekezo la uteuzi wa mkaguzi katika Mkutano huu kwa majadiliano na kuidhinisha.

Taarifa ya Mahesabu imeainishwa katika ukurasa wa 23 hadi 27, ambapo imeandaliwa vizuri na kuidhinishwa na Bodi katika Mkutano maalum uliofanyika tarehe 27/05/2023 na kusainiwa na wajumbe wafuatao:

| | |
|---|---|
| ........................................................ | ........................................................ |
| Bw. Fortunatus M. Magambo | Pro. Lucian Msambichaka |
| **Mkurugenzi** | **Mkurugenzi** |
| Tarehe:27/05/2023 | Tarehe:**27/05/2023** |

## UTHIBITISHO WA MKUU WA IDARA YA UHASIBU

Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Mahesabu (NBAA) kulingana na uwezo wake katika kuwapima na kusajili Wahasibu na wakaguzi wa mahesabu pamoja na sheria ya makampuni namba thelathini na tatu (33) ya mwaka 1972, na kurekebishwa na sheria namba mbili (2) ya mwaka 1995, inaitaka Taarifa ya mahesabu kuambatanishwa na uthibitisho kutoka kwa Mkuu wa Kitengo cha Fedha/ Mahesabu aliyehusika kuandaa taarifa ya Fedha ya Kampuni husika. Mtaalam wa Mahesabu anapaswa kuwasaidia Wakurugenzi/ Wafanyakazi kutekeleza jukumu la kuandaa taarifa za kifedha za taasisi inayotoa picha halisi ya Kampuni na utendaji wake kulingana na Viwango vya Uhasibu vya Kimataifa na matakwa ya kisheria ya uandaaji wa taarifa za kifedha. Jukumu kamili la kisheria kwa utayarishaji wa taarifa za kifedha liko kwa Bodi ya Wakurugenzi kama ilivyoonyeshwa hapo juu kwenye Wajibu wa Wakurugenzi.

Mimi Joel Chikoma, nikiwa ni Mkuu wa idara ya Uhasibu ya TCCIA INVESTMENT PLC ninathibitisha kwamba, Taarifa ya Mahesabu ya mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Desemba, 2022 imeandaliwa kulingana na viwango vya Uhasibu na matakwa ya Kisheria. Ninathibitisha kwamba, Taarifa ya Mahesabu inatoa picha kamili ya TCCIA INVESTMENT PLC kufikia tarehe hiyo iliyotajwa hapo juu na kwamba zimeandaliwa kulingana na taarifa za kifedha zinazotunzwa vizuri.

**Joel Chikoma**
Mkuu wa Idara ya Uhasibu na Uwekezaji
NBAA Membership No: ACPA 3285
Tarehe:**27/05/2023**

# MAHESABU YALIYOKAGULIWA KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHA 31/12/2022

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI YA MWAKA WA FEDHA ULIOISHA 31/12/2022

| | 2022 Shilingi '000 | 2021 Shilingi '000 |
|---|---|---|
| Mapato | 2,997,973 | 2,690,726 |
| Mapato anuwai | 256,091 | 200,183 |
| Mapato mengine/ (hasara) ya uendeshaji | 154,457 | 36,952 |
| Matumizi ya uendeshaji | (1,072,564) | (1,014,150) |
| **Faida ya uendeshaji** | 2,335,957 | 1,913,711 |
| Gharama za mtaji | (349,966) | (374,670) |
| **Faida/ (hasara) kabla ya kodi** | 1,985,991 | 1,539,041 |
| Kodi | (26,181) | (209,182) |
| **Faida/(Hasara) kwa mwaka** | 1,959,810 | 1,329,859 |
| **Mapato mengine kamili** | | |
| Kupanda/ (kushuka) kwa thamani ya hisa | 3,839,666 | (58,088) |
| **Mapato/(hasara) mengine ya mwaka** | 3,839,666 | (58,088) |
| **Jumla ya mapato/(hasara) kwa mwaka** | 5,799,476 | 1,271,771 |
| **Mapato kwa kila hisa** | 26.86 | 18.22 |

## TAARIFA YA WARAKA WA MIZANIA HADI TAREHE 31/12/2022

| Rasilimali | 2022 Shilingi' 000 | 2021 Shilingi' 000 |
|---|---|---|
| **Rasilimali za muda mrefu** | | |
| Mali ya kudumu inayogusika | 117,257 | 139,447 |
| Haki ya matumizi ya rasilimali | 31,050 | 3,256 |
| Uwekezaji wa kwenye ardhi/majengo | 221,347 | 221,347 |
| Uwekezaji wa kwenye hisa | 19,620,534 | 15,253,840 |
| Dhamana za serikali | 13,589,143 | 12,985,104 |
| Rasilimali zisizogusika | 3,000 | 4,500 |
| Amana za makampuni/mashirika | 150,000 | - |
| Uwekezaji mwingine | - | - |
| | **33,761,065** | **28,607,494** |
| **Rasilimali za muda mfupi** | | |
| Rasilimali za biashara | 605,431 | 589,870 |
| Kodi ya muda mfupi | 286,996 | 242,682 |
| Mikopo | 32,994 | - |
| Fedha na thamani ya fedha | 530,185 | 1,011,299 |
| | **1,455,606** | **1,843,851** |
| **Jumla ya Rasimali** | **35,216,671** | **30,451,345** |
| **Mtaji na Madeni** | | |
| **Mtaji** | 2,167,952 | 2,167,952 |
| Jumla ya akiba | 8,883,288 | 5,327,762 |
| Faida kuu | 21,277,811 | 19,908,600 |
| | **32,329,051** | **27,404,314** |
| **Madeni ya muda mrefu** | | |
| Mkopo wa muda mrefu | 2,157,861 | 2,396,962 |
| Kodi iliyoahirishwa | 1,784 | 23,890 |
| | **2,159,645** | **2,420,852** |

| Rasilimali | 2022 Shilingi' 000 | 2021 Shilingi' 000 |
|---|---|---|
| **Madeni ya muda mfupi** | | |
| Madeni ya biashara | 127,863 | 132,095 |
| Dhima ya kukodisha | 30,603 | - |
| Mkopo wa muda mfupi | 239,081 | 209,231 |
| Gawio | 330,428 | 284,853 |
| | **727,975** | **626,179** |
| **Jumla ya madeni** | **2,887,620** | **3,047,031** |
| **Jumla ya mtaji na madeni** | **35,216,671** | **30,451,345** |

**TAARIFA YA WARAKA WA MIZANIA HADI TAREHE 31/12/2022**

Taarifa hii ya mahesabu ilithibitishwa kwa ajili ya kutangazwa na Bodi na ilisainiwa kwa niaba yao na:

..........................................................

Bw. Fortunatus M. Magambo
**Mkurugenzi**
Tarehe:27/05/2023

..........................................................

Pro. Lucian Msambichaka
**Mkurugenzi**
Tarehe:**27/05/2023**

# TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA MWAKA 2022

| | Mtaji wa hisa | Mapato ya hisa | Jumla ya mtaji wa hisa | Akiba ya thamani ya uwekezaji kwenye hisa | Gharama ya IPO | Faida kuu | Jumla ya mtaji |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Shilingi '000 | '000 | '000 | '000 | '000 | '000 | '000 |
| **Mwaka uliopita** | | | | | | | |
| **Usawa tarehe 31/12/2021** | **1,459,153** | **708,799** | **2,167,952** | **6,655,287** | **(629,662)** | 18,972,205 | **26,571,007** |
| **Faida ya mwaka** | | | | | | 1,329,859 | 1,329,859 |
| **Mapato mengine** | | | | 58,088 | - | - | 58,088 |
| **Kuhamisha kwenda akiba kuu** | | | | (45,000) | | (45,000) | - |
| **Gawio** | | | | | | (438,464) | (438,464) |
| **Usawa tarehe 31/12/2022** | 1,459,153 | 708,799 | 2,167,952 | 5,957,424 | (629,662) | 19,908,600 | 27,404,314 |
| **Muda wa sasa:** | | | | | | | |
| **Usawa tarehe 31/12/2021** | **1,459,153** | **708,799** | **2,167,952** | **5,957,424** | **(629,662)** | **19,908,600** | **27,404,314** |
| **Mapato ya mwaka** | | | | | | 1,959,810 | 1,959,810 |
| **Mapato mengine** | | | | 3,839,666 | | 3,839,666 | 3,839,666 |
| **Kuhamisha kwenda akiba kuu** | | | | (284,140) | | (284,140) | |
| **Gawio** | | | | | | 729,577 | 729,577 |
| **Usawa tarehe 31/12/2022** | **1,459,153** | **708,799** | **2,167,952** | **19,512,950** | **(629,662)** | **21,777,811** | **32,299,051** |

# TAARIFA YA MZUNGUKO WA FEDHA

| | 2022 | 2021 |
|---|---|---|
| **Mzunguko wa fedha kutokana na uendeshaji** | **Shilingi '000** | **Shilingi '000** |
| Fedha iliyotoka kwenye shughuli za uendeshaji | 2,080,332 | 1,908,698 |
| Gharama za kifedha | (349,966) | (374,670) |
| Kodi iliyolipwa | (92,602) | (157,880) |
| **Fedha taslimu inayotokana na uendeshaji** | **1,637,764** | **1,376,148** |
| **Mzunguko wa fedha kutokana na uwekezaji** | | |
| Manunuzi ya mali ya kudumu inayogusika | (10,567) | (142,192) |
| Manunuzi ya Haki ya kutumia Rasilimali | (57,323) | - |
| Manunuzi ya Rasilimali Isiyogusika | - | (6,000) |
| Mzunguko kwenye uwekezaji katika hisa | (527,028) | (463,814) |
| Manunuzi ya amana za serikali | 604,039 | 593,071 |
| Mzunguko kwenye amana za makampuni | 10,000 | 10,000 |
| Mikopo | 61,728 | - |
| Faida/(Hasara) kwenye uuzaji wa hisa | 154,457 | 36,952 |
| **Fedha taslimu iliyotumika katika uwekezaji** | **(1,256,228)** | **28,017** |
| Mzunguko wa mkopo | (209,251) | (183,094) |
| Mzunguko wa dhima ya kukodisha | (30,603) | (39,093) |
| Gawio lililolipwa | (684,002) | (376,912) |
| **Fedha taslimu iliyotokana na mtaji** | **(862,650)** | **(599,099)** |
| **Jumla ya fedha taslimu za mzunguko kwa mwaka** | **(481,114)** | **805,066** |
| Fedha na thamani ya fedha mwanzo wa mwaka | **1,011,299** | **206,233** |
| **Fedha na thamani ya fedha mwisho wa mwaka** | **530,185** | **1,011,299** |

Dondoo Na. 18/5/2023

# WASILISHO

**WASILISHO:**

Ndugu Wanahisa mnaombwa kupokea na kuridhia Taarifa ya Wakurugenzi na Taarifa ya Fedha iliyokaguliwa kwa kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2022 na kuazimia kama ifuatavyo.

## Azimio la 2/2023

Taarifa ya Mwaka ya Wakurugenzi na Taarifa ya Fedha iliyokaguliwa kwa kipindi cha Mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2022 imepitishwa kama ilivyowasilishwa.

# KUTANGAZA GAWIO

## KUTANGAZA GAWIO


Kwa mwaka wa fedha ulioshia Desemba, 31 2022, Bodi inapendekeza kulipa gawio la shilingi 13 kwa hisa (2021: shilingi 10 kwa hisa).

## WASILISHO

Bodi inapendekeza kuwa kama Mkutano Mkuu utaridhia pendekezo hili, malipo ya gawio kwa wanahisa yafanyike baada ya kupitisha azimio hili. Kwa wanahisa ambao wana akaunti za benki malipo yatalipwa kupitia kwenye akaunti zao na kwa njia ya mitandao ya simu.

## Azimio la 3/2023

Mkutano Mkuu umeazimia, kuridhia pendekezo hili kwamba gawio la shilingi za Kitanzania Kumi (13) kwa kila hisa kama ilivyopendekezwa na Bodi ya Wakurugenzi.



## UTEUZI WA MKAGUZI WA MAHESABU YA KAMPUNI KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA DESEMBA 31, 2022

Kama ilivyoelezwa kwenye Taarifa ya Mahesabu ya Kampuni kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Desemba 31, 2022, Mahesabu ya Kampuni yalikaguliwa na Kampuni ya Ukaguzi wa Mahesabu na Ushauri ya CROWE Tanzania. Hadi sasa Bodi imeridhika na kazi ambayo ilifanywa na Kampuni hii kwa mwaka 2022. Aidha Kampuni hiyo imeonyesha nia ya kuendelea kukagua Mahesabu ya Kampuni yetu kama watateuliwa tena.

### WASILISHO

Bodi inapendekeza kuwa CROWE Tanzania wateuliwe tena kukagua Mahesabu ya Kampuni kwa mwaka unaoishia Desemba 31, 2023. Ada ya ukaguzi inayopendekezwa ni kiasi cha Shilingi 20 milioni Kabla ya kodi. Ada inayopendekezwa na Bodi imezingatia mwenendo wa Soko kwa taaluma ya Uhasibu na Ukaguzi, ukuaji wa shughuli za Kampuni na mfumuko wa bei nchini.

## Azimio la 4/2023

Imeazimiwa kukubaliana na pendekezo la Bodi ya Wakurugenzi kuwa CROWE Tanzania waendelee kukagua Mahesabu ya Kampuni kwa Mwaka wa Fedha unaoishia Desemba 31, 2023. Pamoja na kuidhinisha Shilingi 20 milioni kabla ya kodi kama gharama za malipo ya ukaguzi wa Mahesabu ya Kampuni.

## PENDEKEZO KUHUSU MALIPO YA WAKURUGENZI

Malipo ya Wajumbe wa Bodi, [Directors fees] yameainishwa kwenye Katiba ya Kampuni. Kifungu Namba 70 [i] kinaeleza kuwa: "The remuneration of the Directors shall from time to time be determined by the Company in General Meeting".


Malipo haya huwa yanawekwa kwenye Bajeti ya Kampuni kila mwaka. Malipo ya Wajumbe yanatokana na ukweli kuwa Wajumbe wa Bodi hutumia muda mwingi kusimamia shughuli za Kampuni, badala ya kusimamia shughuli zao binafsi. Ikumbukwe kuwa Wajumbe wa Bodi ndio wanawajibika kwa Mkutano Mkuu kwa kusimamia shughuli za Kampuni kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Makampuni ya Mwaka 2002, pamoja na kanuni na taratibu zilizowekwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) na Soko la Hisa la Dar-es-Salaam, utawala bora na ufanisi wa Kampuni. Kwa kifupi chini ya Sheria ya Makampuni, Wajumbe wanawajibika kuhakikisha kuwa wanasimamia vema Kampuni ili wanahisa wasipoteze fedha zao na kwamba mtaji wa Kampuni unakua.

### WASILISHO

Kwa kuzingatia matokeo ya shughuli za Kampuni kwa Mwaka wa fedha utakaoishia Desemba 31, 2023 , Menejimenti inapendekeza kuwa Wajumbe wa Bodi walipwe Shilingi milioni nne na laki nane (Shilingi 4,800,000). Kama ilivyokuwa mwaka jana.

## Azimio la 5/2023

Imeazimiwa kwamba kama ilivyopendekezwa na Menejimenti, malipo ya Wakurugenzi wa Bodi yawe Shilingi milioni nne na laki nane (Shilingi 4,800,000) kwa kila Mjumbe wa Bodi.



Dondoo Na. 18/9/2023

## KUPOKEA, KUJADILI NA KURIDHIA PENDEKEZO LAKUBADILISHA JINA LA KAMPUNI

**WASILISHO**

Bodi inapendekeza mabadiliko makubwa katika nembo na jina la kampuni. Bodi inaamini kuwa mabadiliko haya ni muhimu ili kuimarisha utambulisho wetu, kuzoea mwenendo unaobadilika katika soko, na kupata fursa mpya za biashara.

**SABABU ZA MABADILIKO:**

**KUBORESHA NA KUIMARISHA CHAPA:** Nembo na jina letu la sasa huenda havina uwezo wa kuakisi kikamilifu maono, thamani, na nafasi ya kampuni katika soko. Nembo mpya na iliyoimarishwa inaweza kutusaidia kuwasilisha mtazamo wetu wa ubunifu na wa kufikiria mbele.

**FAIDA YA USHINDANI:** Nembo na jina jipya vinaweza kutupa ushindani kwa kutufanya tuwe tofauti, washirika, na wawekezaji watarajiwa. Itatusaidia kusimama kati ya ushindani mkubwa katika soko.

**ULINGANIFU NA SOKO:** Ni muhimu kwetu kubadilika kulingana na mabadiliko haya na kuhakikisha kuwa nembo na jina letu linaelekea kwa hadhira yetu ya lengo. Hii itatusaidia kuendelea kuwa na umuhimu na kuwavutia wawekezaji wengi zaidi.

**UPANUZI NA UKUAJI**: Ikiwa tunazingatia kupanua wigo wetu wa bidhaa, kuingia katika masoko mapya, au kubadilisha biashara zetu, mabadiliko ya nembo na jina yanaweza kuwezesha mipango mikakati hiyo. Itatuwezesha kuanzisha kitambulisho kipya kinacholingana na malengo yetu ya baadaye.

**WASILISHO:**

Bodi inapendekeza kwa Mkutuno Mkuu kama ifuatavyo;

JINA JIPYA LA KAMPUNI**: AFRIPRISE INVESTMENT PLC.**

**NEMBO MPYA:**

# Azimio la 6/2023

Imeazimiwa jina jipya la Kampuni liwe hilo **AFRIPRISE INVESTMENT PLC.**

## KUPOKEA, KUJADILI NA KURIDHIA PENDEKEZO LA KUTOA HISA STAHIKI

Wapendwa Wanahisa Bodi ya Wakurugenzi, imepokea pendekezo kutoka kwa wanahisa la kutoa hisa stahiki (rights issue share offering). Baada ya kutathmini na kwa ushauri wa timu yetu ya uongozi na wataalam, tunaamini kwamba fursa hii itatoa uwezo mkubwa wa kuongeza thamani kwa wanahisa na kuimarisha mtaji wa kampuni yetu.

### SABABU ZA KUTOA HISA KWA NJIA YA HISA STAHIKI

**BEI YA KUVUTIA YA UNUNUZI:** kununua hisa zaidi kwa bei nzuri ya ununuzi ya Shillingi 145/= kwa kila Hisa.
**KULINDA ASILIMIA YA UMILIKI:** Kwa kushiriki katika kununua hisa stahiki, Mwanahisa anapata fursa ya pekee ya kuendeleza asilimia yake ya umiliki katika kampuni na kulinda maslahi yake naushawishi wake.
**KUONGEZA UKUAJI NA KUUNDATHAMANI:** Mtaji utakaopatikana utaelekezwa kwenye vyanzo vipya mapato kwa gharama ya chini ya mtaji. Hatua hii itasaidia kufikia malengo yetu ya ukuaji na kuongeza thamani kwa wanahisa wote kama ifuatavyo:


**KUONGEZA UKWASI:** Kutoa hisa kwa njia ya hisa stahiki kutasababisha ongezeko la idadi ya hisa zilizopo, hivyo kuimarisha ukwasi wa hisa za kampuni yetu kwenye soko.

**KUPATA MTAJI WA HISA:** Lengo kuu la kutoa hisa kwa njia ya hisa stahiki ni kupata kiwango kikubwa cha mtaji wa hisa, kiasi cha Shillingi 10,578,860,700/= (kabla ya kutoa gharama). Fedha hizi zitatumiwa kwa ustadi kukuza uwekezaji wa Kampuni.

**KUONGEZA MALI:** Kwa kuwekeza mapato yatakayokana na kutoa hisa stahiki katika, maeneo mengine ndani na nje ya Tanzania, lengo letu ni kuongeza ukuaji wa kiuchumi wa Kampuni yaani kusababisha ukuaji wa muda mrefu na ufanisi wa uendeshaji.

**KUFIKIA MALENGO YA MKAKATI:** Kutoa hisa kwa njia ya stahiki kutawezesha kufikia malengo yetu ya kupata mtaji ndani ya muda wa bajeti iliyopangwa, na kusukuma Kampuni yetu kuelekea mafanikio makubwa zaidi.

### WASILISHO
Tunafuraha kuwasilisha pendekezo la kutoa hisa stahiki za kawaida na kuomba idhini yenu kwa hatua hii.



## Azimio la 7/2023

Imeazimiwa kuwa Kampuni itaanzisha kutoa hisa kwa njia ya stahiki kwa kutoa hisa mpya 72,957,660 kwa Shillingi 145/= kwa kila Hisa. Kila mwanahisa anayemiliki Hisa za kawaida atakuwa na haki ya kununua Hisa moja Mpya kwa kila Hisa moja ya kawaida aliyonayo siku ya kumbukumbu.

| No | Majina ya Wanahisa | Hali |
|---|---|---|
| 1 | PUBLIC SERVICE SOCIAL SECURITY FUND | Wanahisa |
| 2 | MKOMBOZI FISHING & MARING TRANSPORT LTD | Wanahisa |
| 3 | ABBASI EXPORTS LIMITED | Wanahisa |
| 4 | CHRISTOPHER MWITA GACHUMA | Wanahisa |
| 5 | NIMROD ELIREHEEMAH MKONO | Wanahisa |
| 6 | ZUMBI ELVIS MUSIBA(ADMIN) ELVIS ARISTABLUS MUSIBA(DECEASED) | Wanahisa |
| 7 | JAMES MAJUKANO GEGE | Wanahisa |
| 8 | ABIHUDI SAULO MHIDZE | Wanahisa |
| 9 | JULIUS MATIKO MWITA | Wanahisa |
| 10 | TESE & TECHE ENGINEERING LTD | Wanahisa |
| 11 | DONALD OBADIA MUSHI | Wanahisa |
| 12 | AMBROSE L MSIGWA(ADMIN) LUKENGELO WILFRED MSIGWA (DECEASED) | Wanahisa |
| 13 | TCCIA HQ | Wanahisa |
| 14 | ABERHARD JOHN MBEPERA | Wanahisa |
| 15 | MASUKA VILLAGE HOTEL LTD | Wanahisa |
| 16 | WILLIAM EDWARD MKENDA | Wanahisa |
| 17 | DR. JOSHUA BARIYE AMO | Wanahisa |
| 18 | EVANS EDDY MLAY | Wanahisa |
| 19 | TCCIA TANGA | Wanahisa |
| 20 | MICHAEL DANIEL KAVUTA | Wanahisa |
| 21 | SEBASTIAN JOSEPH KUNJUMU | Wanahisa |
| 22 | LWIHURA ZAKAYO KACHECHEBA | Wanahisa |
| 23 | ESTHER MASATU FUNDI | Wanahisa |
| 24 | ZAID BARAKA KASIM | Wanahisa |
| 25 | JULLIAN WILLIAM KHAMBAYTA | Wanahisa |
| 26 | NATHAN EDWARD MNYAWAMI | Wanahisa |
| 27 | HAROLD ENOCK TEMU | Wanahisa |
| 28 | KINONI ADAM WAMUNZA | Wanahisa |
| 29 | THOMAS RUGUMBA GHATI | Wanahisa |
| 30 | DR. DOROTHY MARTIN MASOZA | Wanahisa |
| 31 | KANYENYE KISULILA MATANGA | Wanahisa |
| 32 | JOSEPH ELISHA LEMBO | Wanahisa |
| 33 | SWEDI RAMADHANI KAITABA | Wanahisa |
| 34 | JOEL TIMOTH CHIKOMA | Wanahisa |
| 35 | GODEBERTA LAURENT KALEMERA | Wanahisa |
| 36 | LUSAJO TELATELA | Wanahisa |
| 37 | BEATRICE ZACHARY OMACH | Wanahisa |
| 38 | MARY L MTAVANGU | Wanahisa |
| 39 | KEVIN GOSBERT KABENGULA | Wanahisa |
| 40 | MOHAMED KHAMIS KIMBAU | Wanahisa |

| | | |
|---|---|---|
| 41 | SAMWEL FREDERICK MANDARA | Wanahisa |
| 42 | KENNEDY NELSON SIMUNDI | Wanahisa |
| 43 | VALLERIA POTAMI MANDE | Wanahisa |
| 44 | FRANCIS PAUL MGAYA | Wanahisa |
| 45 | CHARLES PARADISO URASA | Wanahisa |
| 46 | JOSEPHINE ERNEST MHINA | Wanahisa |
| 47 | ROGACIAN AUGUST MASSAWE | Wanahisa |
| 48 | RAHEL MHUMPA | Wanahisa |
| 49 | KAMTECH ENTERPRISES | Wanahisa |
| 50 | ISHMAEL SAGIRAKI LAISER | Wanahisa |
| 51 | AHMAD HASHIMU NAMWADILANGA | Wanahisa |
| 52 | REGINA LAWRENCE MSUSA | Wanahisa |
| 53 | JACKSON TAIRI NYAKUYEYA | Wanahisa |
| 54 | ADAM ABDALA ZUKU | Wanahisa |
| 55 | IRENE BAHOYA KULOLA | Wanahisa |
| 56 | RUKIA MAKARANGA | Wanahisa |
| 57 | MASIMBA CLEMENT KAKA | Wanahisa |
| 58 | JAMES SIONGO NYAKIBALI | Wanahisa |
| 59 | BERTHA BIANCA KIMAMBO | Wanahisa |
| 60 | BARTHOLOMEW MAJOR KUNZUGALA | Wanahisa |
| 61 | GAMALIELI ISSAC NYAMBACHA | Wanahisa |
| 62 | DOREEN SEMALI KISAMO | Wanahisa |
| 63 | DOMINIC LUSASI | Wanahisa |
| 64 | CHORRAY THOMAS | Wanahisa |
| 65 | HELLENA BUNEBUNE BULAMILE | Wanahisa |
| 66 | OLYPAH MALELE HAULE | Wanahisa |
| 67 | YUSTA EDWARD SAILALE | Wanahisa |
| 68 | BONITA MWITA MATIKO | Wanahisa |
| 69 | THECLA WILSON MWITA | Wanahisa |
| 70 | ALI MOHAMED SANGAL | Wanahisa |
| 71 | DEOGRATIUS ANDREW CHUWA | Wanahisa |
| 72 | MASAIDA MUSSA CHIWINGA | Wanahisa |
| 73 | DEUSDEDIT TUNGI MANGWALA | Wanahisa |
| 74 | SAID HUSEIN SEIF | Wanahisa |
| 75 | DOMINIC DANIEL KYARUZI | Wanahisa |
| 76 | MUSA ALFRED RAPHAEL | Wanahisa |
| 77 | MAGRETH MERCHIOR MANGO | Wanahisa |
| 78 | NGIKANIAWO GEOFREY LYIMO | Wanahisa |
| 79 | KELVIN MATHIAS MASUNGA MASENDE | Wanahisa |
| 80 | RENDI COMPANY LTD | Wanahisa |

| | | |
|---|---|---|
| 81 | AMBROSE REMMY MWAKIMBWALA | Wanahisa |
| 82 | GRACE SILYA JONATHAN | Wanahisa |
| 83 | PETER WILLIAM KIFUNGUOMALI | Wanahisa |
| 84 | BETHUEL ELINAJA TEMU | Wanahisa |
| 85 | REVOCATUS BELLE RUMISHA | Wanahisa |
| 86 | ARELLA RABBIEL MWASHA | Wanahisa |
| 87 | SHARON ELLY | Wanahisa |
| 88 | ANTHONY ALBERTO DOBEYE | Wanahisa |
| 89 | DANIEL WILSON CHARO | Wanahisa |
| 90 | JAVAN MUGANDA PERE | Wanahisa |
| 91 | BARKE LUCAS MWAKALINGA | Wanahisa |
| 92 | DEOGRATIAS ATHANAS MROSSO | Wanahisa |
| 93 | NEDUVOTO PINIEL MOLLEL | Wanahisa |
| 94 | ROSE REUBEN MWAISAKA | Wanahisa |
| 95 | THOMAS PINIEL MEMIRIEK | Wanahisa |
| 96 | ISABELA BEDA LYIMO | Wanahisa |
| 97 | SHAMSI K MUSSA | Wanahisa |
| 98 | KELVIN IVOD MATHIAS MOSHA | Wanahisa |
| 99 | CLAUDI COSMAS MFUNGO | Wanahisa |
| 100 | LEONARD JOSIAJ SHIMWELA | Wanahisa |
| 101 | AMAN EDWARD STEPHEN | Wanahisa |
| 102 | WIDALA BARNABA NDEZI | Wanahisa |
| 103 | JOSEPH KIMARIO PHILEMO | Wanahisa |
| 104 | RONALD KATO | Wanahisa |
| 105 | MICHAEL DEOGRATIUS MKANGI | Wanahisa |
| 106 | PETER JOHN LISUNGU | Wanahisa |
| 107 | ISSA JUMA ISSA | Wanahisa |
| 108 | INNOCENT FAHAMUEL NKURWA | Wanahisa |
| 109 | AZIZA JUMA MOHAMED MATOLA | Wanahisa |
| 110 | HOOD HAMZA SALIM | Wanahisa |

# KUFUNGA MKUTANO MKUU WA KUMI NA NANE



**TCCIA INVESTMENT PLC**

**P.O.Box 72678,**
**Dar es Salaam, Tanzania**
**Mobile: +255 684 535 545**
**Email: info@tcciainvestment.com,**
**Web site: https://www.tcciainvestment.com**